*Mulika, Juz. 44(2), 248-267*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

# Wahusika wa Kivisasili na Athari yake katika Riwaya ya Kiswahili

*Rose Jackson Mbijima*[1]

DOI: https://doi.org/10.56279/mulika.na44t2.6

**Ikisiri**

Wahusika ni kipengele muhimu cha kazi yoyote ya fasihi. Umuhimu wake unatokana na ukweli kwamba ujitokezaji wa vipengele vingine vya msingi vya fani na maudhui katika fasihi hutegemea sana namna ambavyo mwanafasihi amewaumba wahusika wake. Makala imetumia riwaya teule tatu ambazo ni *Nagona*, na *Mzingile* za Euphrase Kezilahabi na *Ziraili na Zirani* ya William Mkufya. Kwa hiyo, makala imejikita kuwabainisha wahusika wa kivisasili kwa kuzielezea sifa zao za msingi zinazowatofautisha na wahusika wasio wa kivisasili. Wahusika wa kivisasili waliobainishwa ni pamoja na Kakulu, Mimi, Kizee, Ziraili, Zirani na Kinjeketile Ngwale. Aidha, makala imejadili athari ya wahusika hao katika riwaya teule. Kwa kutumia Nadharia ya Uheminitiki, tumebaini athari anuwai. Mathalani, wahusika wa kivisasili waliotumika katika riwaya wamewezesha urithishaji wa amali za kiutamaduni na uhistorishaji. Pia, wahusika hawa wana athari ya uunganishaji wa ujadi na usasa. Vilevile, wanawezesha utambulishaji wa jamii husika.

## 1.0 Utangulizi

Wataalamu mbalimbali wa kale na wa sasa wamefasili visasili. Wataalamu wa kale ni pamoja na Ruskin (1869) anayefasili visasili kwamba ni hadithi zenye maana ya ziada inayohusishwa nazo mbali na maana yake ya asili. Kisasili kuwa na maana ya ziada inayohusishwa nacho kunatokana na ukweli kwamba kinajengwa katika mazingira yasiyo ya kawaida ambayo binadamu hajayazoea. Mara nyingi, hadithi za namna hii zinahusisha wahusika ambao ni viumbe wasio wa kawaida. Mtaalamu mwingine aliyefasili visasili ni Bascom (1965) ambaye ana mtazamo sawa na Ruskin (1869) kuhusu wahusika wa visasili kwamba ni viumbe visivyo vya kawaida japo yeye anaongeza kuwa, wakati mwingine, wahusika hao wanaweza pia kuwa ni mashujaa wa zamani.

Akiibua mawazo tofauti na yale ya Ruskin (1869), mwanafalsafa wa Kifaransa, Cassirer (1946, 1953), anaona kuwa visasili ni ruwaza au mwelekeo wa awali wa

[1] Mhadhiri Mwandamizi, Idara ya Lugha na Fasihi, Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania, Baruapepe: rosembijima2019@gmail.com; rose.mbijima@duce.ac.tz

mawazo ya binadamu. Pia, mawazo kama haya tunayapata kwa Breslauer (1997) na Schwartz (2004). Binadamu anautambua na kuuelewa ulimwengu kwa kutumia mifumo ya ishara. Visasili hutumia lugha za kiishara ambazo zinaweza kutumika kutoa mafunzo kwa ulimwengu na walimwengu pia (Cassirer 1946, 1953; Levi-Strauss, 1963). Kinachojidhihirisha katika fasili hii ni kwamba Cassirer anadokeza jinsi visasili vinavyohusiana na lugha ya kiishara.

Murray (1960) anaeleza kwamba ni dhahiri kuwa visasili vina sifa bainifu ambazo zinafafanua hali au tukio muhimu la kawaida au lisilo la kawaida linalohusiana na kuwapo kwa binanadamu katika ulimwengu. Hivyo, kisasili ni masimulizi yenye athari inayoweza kudhihirika katika mawanda ya jamii nzima. Mwanahistoria Yerushalmi (1982) ana mawazo mapana zaidi kuhusu visasili. Anabainisha kuwa visasili ni masimulizi kuhusu mambo yaliyopita ambayo yanaleta kumbukumbu ya dhati, takatifu na jumuishi kwa kundi fulani la watu.

Magoulick (2000) anasema kuwa visasili, hueleza namna mhusika anavyopita katika matukio yanayopangwa. Kwa hiyo, visasili ni utanzu wa fasihi ambao una sifa tofauti na sifa za tanzu nyingine. Anaendelea kueleza kuwa, visasili ni hadithi za zamani za kiishara zinazohusu asili ya ulimwengu, zinaweza kuhusishwa na imani za dini na miviga na kuwa na mchango katika utamaduni fulani. Kwa mujibu wa Magoulick (2000), kuna mambo sita ya msingi ambayo yanajirudia katika karibu fasili zote zinazotolewa na wataalamu mbalimbali wa fasihi kuhusu visasili. Visasili vinaweza kufasiliwa kwa namna yoyote ile ilimradi mambo hayo yazingatiwe. Mambo hayo ni yafuatayo:

Kwanza, visasili ni masimulizi kuhusu asili ya ulimwengu na walimwengu japo katika mazingira mengine vinaweza kuwa mahususi kwa jamii au utamaduni fulani. Kwa kuwa vinahusishwa na ulimwengu, muundo wake ni wa kikale, yaani wa zamani wakati wa kuumbwa kwa ulimwengu. Wahusika wake ni wanadamu wa asili au mizimu na miungu. Pili, visasili ni masimulizi kuhusu uungu na mara nyingi vinahusishwa na miviga. Masimulizi hayo yana msingi wake katika imani za dini. Vinaaminika kuwa ni vya kweli japokuwa ukweli huo unakuwa ni wa kisitiari zaidi kuliko kiuhalisia. Katika jamii moja kunaweza kuwa na visasili vya kiungu na vya kidunia kwa wakati mmoja. Tatu, visasili ni masimulizi yanayoakisi mfumo na desturi katika utamaduni wa jamii husika.

Nne, visasili ni masimulizi yanayowasilisha epistimolojia, yaani namna ya kuelewa asili kwa kupangilia mawazo. Kwa mfano, wanamuundo wanatambua pacha mbili zinazopingana, kama mwanga na giza, ukweli na uongo, wema na ubaya kuwa ni mambo ya msingi katika visasili. Tano, masimulizi ya visasili mara nyingi yanahusisha mashujaa, wanadamu wa asili, majitu, mizimu na miungu ambao wanaaminika kusababisha majanga mbalimbali yanayotuunganisha na ukweli kuhusu maisha au kuanzisha ruwaza za maisha ya binadamu. Sita, visasili

ni masimulizi ambayo yanabadili au yanashindana na ukweli. Huonesha wahusika na matukio ambayo yanashangaza, kufadhaisha na kustaajabisha, maagano, mapatano, mila, desturi na jadi za kila siku za jamii.

## 2.0 Dhana na Sifa za Wahusika wa Kivisasili katika Riwaya

Sehemu hii inajadili mambo mawili, dhana ya wahusika kwa jumla na sifa za wahusika wa kivisasili. Tunaanza na dhana ya wahusika kwa jumla.

### 2.1 Dhana ya Wahusika

Wahusika ni viumbe wa kisanaa wanaopatikana katika kazi yoyote ile. Wanabuniwa kutokana na mazingira na malengo ya msimulizi. Viumbe hawa huwa sehemu ya kazi nzima. Pia, wahusika binadamu wanaopatikana katika kazi ya kifasihi wana sifa za kimaadili, kitabia, kiitikadi, kifalsafa na ambazo hutambulishwa na wanayoyasema (mazungumzo) na wanayoyatenda (matendo). Wahusika huweza kutambulishwa pia na maelezo ya mhusika au msimulizi (Wamitila, 2002). Wahusika wa kazi za kifasihi wamechunguzwa na wataalamu mbalimbali. Wataalamu hao wanaeleza kuwa wahusika ni kipengele muhimu cha fani (Msokile, 1992; Njogu na Chimerah, 2008).

Hivyo, katika kazi yoyote ya fasihi, riwaya ikiwamo, wahusika ni kipengele cha msingi. Hii ni kutokana na umuhimu wao mkubwa katika kuiunda simulizi ya kifasihi. Wahusika wanaweza kuathiri simulizi inayosimuliwa kwa kupeleka mbele matukio katika simulizi. Wahusika hawa, hushabihiana na watu kwa kuwa fasihi huandikwa kwa ajili ya watu na, kwa hiyo, huwahusu watu hao. Kwa kawaida, wahusika si watu halisi, bali ni matokeo ya ubunifu wa msanii ili kuakisi masuala kadhaa ya kijamii ambayo msanii ameyakusudia. Wahusika ni viumbe wa kubuni wanaotokana na fantansia, mwigo na kumbukumbu: “... ni watu bandia wasio na damu na nyama… Mhusika si binadamu halisi lakini anafanana na binadamu. Hana akili, haiba, itikadi wala uwezo wa kutenda bali ana sifa zinazotuwezesha kumtolea maelezo ya kisaikolojia na kiitikadi” (Bal; 1997: 115).

Kwa hiyo, uhusika ni kipengele cha msingi katika riwaya, kwani kila tukio lipo ili kumfafanua mhusika na maendeleo yake. Mhusika ni kitu kilichochorwa kwa fikra (maneno) kwa msingi wa vielelezo vya kitamaduni, kwa maana kwamba mhusika wa fasihi ya jamii fulani ataeleweka vizuri na kwa uhakika zaidi na jamii hiyo husika (Madumulla, 2009). Pia, Madumulla (2009) akiwarejelea Kasper na Wuckel (1982) anaeleza kuwa mhusika ni picha ambayo huchorwa na fasihi na kiini cha vitu vyote vipya, dhamira na mada za fasihi.

### 2.2 Sifa za Wahusika wa Kivisasili

Wahusika wa kivisasili wana sifa nyingi, baadhi ya sifa zao zinafanana na sifa za mhusika wa kiutendi au shujaa. Sifa ya kwanza ni kuzaliwa kiajabuajabu, kama vile kupitia mguuni badala ya njia ya kawaida ya uzazi, kuzaliwa na mvi kichwani,

kuongea mara tu baada ya kuzaliwa, kutembea mara tu baada ya kuzaliwa na kuongea wangali bado wapo tumboni. Historia ya maisha yao inagubikwa na mafumbo na miujiza mingi.

Pili, maisha yao huambatana na motifu ya safari ambapo mhusika huondoka nyumbani na kusafiri kwenda mahali pengine. Safari hiyo huambatana na kupitia mambo mengi magumu na ya hatari, vikwazo vingi, majaribu kutoka kwa wafalme wakatili, majitu, bahari za kutisha na miungu. Hata hivyo, hufanikiwa kuanzisha makazi mapya yanayofanana na yale ya mwanzo. Karibu aina zote za safari zina mwanzo unaofanana (Senkoro, 1997). Zipo sababu nyingi zinazowasukuma wahusika kuanzisha safari. Kuna safari zinazofanywa ili kugundua na kuchunguza mambo ya ajabu na ya kuvutia, ugomvi wa kifamilia, kutafuta kitu cha thamani, kutafuta elimu, kufukuzwa kwa sababu za kiutamaduni na uhamisho wa kujitakia. Sababu hizi za kuanzisha safari zinakubalika katika fasihi andishi na simulizi pia (Senkoro, 1997). Kwa mfano, ni jambo la kawaida kwa watoto wa watemi wanapofikia umri fulani kuelekea utu uzima. Hulazimika kuondoka eneo la himaya ya baba zao. Hii ni sheria kwa watoto wa watemi, si jambo la hiari (Sungi, 2011).

Sifa nyingine ya wahusika wa kivisasili ni kwamba mhusika katika kusafiri kwake anakutana na marafiki wanaomuunga mkono na kumsaidia katika kutimiza azma na malengo ya safari yake. Marafiki hao humpa msaada wakati wa majaribu, vikwazo na mateso yanayoweza kumpata. Wakati mwingine anaweza kupata msaada na maelekezo muhimu kuhusu safari yake kutoka kwa miungu wa kike au wa kiume. Hii ni kwa sababu inaaminika kwamba mhusika wa kivisasili ni zawadi ambayo jamii hupewa na miungu. Sifa ya mwisho ni kwamba mara nyingi mhusika wa kivisasili huwa ni wa jinsi ya kiume (Bowra, 1952; Belcher, 1999).

Miongoni mwa kazi za fasihi andishi ya Kiswahili zilizotumia wahusika wa kivisasili ni tamthiliya kama *Jogoo Kijijini* na *Ngao ya Jadi* (Hussein, 1976), na *Lina Ubani* (Mhando, 1984) na riwaya ya *Adili na Nduguze* (Robert, 1952). Mathalani, katika riwaya ya *Adili na Nduguze*, Adili anachanganyikana na hata kuwasiliana na majini (Senkoro, 1982). Kazi zingine ni kama vile riwaya za *Siri Sirini* (Chimerah, 2014), *Mkamandume* (Mohamed, 1976), *Ziraili na Zirani* (Mkufya, 1999) *Nagona* (Kezilahabi, 1990) na *Mzingile* (Kezilahabi, 1991).

## 3.0 Methodolojia

Utafiti huu ni wa maktabani ambapo maktaba zilizohusika ni Maktaba ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Makavazi ya Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI) na Maktaba ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE). Riwaya teule za Kiswahili zilizotumika katika utafiti huu zilichaguliwa kwa kutumia uteuzi wa kimakusudi, mbinu inayomruhusu mtafiti kuchagua riwaya zinazofaa zaidi kwa madhumuni ya utafiti huu. Kwa hiyo,

vigezo vilivyoongoza uteuzi wa riwaya ni pamoja na kuwapo kwa wahusika wanaodhihirisha kwa uwazi mienendo na sifa za wahusika wa kivisasili. Kwa kuzingatia misingi hiyo, riwaya teule zilichukuliwa kama vielelezo mahususi vinavyoweza kutoa uelewa wa kina kuhusu namna waandishi wa Kiswahili wanavyowasawiri wahusika wa kivisasili na athari zao katika riwaya ya Kiswahili. Ukusanyaji wa data za makala hii ulifanyika kwa kutumia mbinu ya usomaji makini wa matini. Mbinu hii ilihusisha usomaji wa nyaraka maktabani, ikiwamo kusoma riwaya teule kwa kina na kwa kurudia, kwa lengo la kubainisha vipengele vinavyojenga taswira ya kivisasili kwa wahusika, ikiwamo matendo yao, kauli na sifa zao kwa jumla, pamoja na athari zao katika riwaya teule. Katika mchakato huu, mtafiti alitenga na kurekodi dondoo mahususi kutoka katika riwaya teule zinazoonesha wazi au kwa njia fiche wahusika wa kivisasili. Mbali na data ya msingi kutoka katika riwaya, makala ilitumia pia data iliyopatikana kwa kusoma matini mbalimbali, ikijumuisha vitabu vya nadharia ya fasihi, makala za kifasihi, tasnifu na tafiti zilizotangulia zinazohusiana na uhusika katika riwaya ya Kiswahili. Data hii ilisaidia kuimarisha misingi ya kinadharia na kuweka uchanganuzi wa riwaya katika muktadha mpana wa mjadala wa kitaaluma. Kwa jumla, mbinu hii ya ukusanyaji wa data ilihakikisha upatikanaji wa taarifa sahihi, zenye kina na zinazohusiana moja kwa moja na lengo la makala hii.

## 4.0 Nadharia ya Uhemenitiki

Kuna wataalamu kadhaa ambao wanahusishwa na uasisi, ukuaji na maendeleo ya Nadharia ya Kihemenitiki. Baadhi yao ni Friedrich Schleiermacher (1768-1834), Wilhelm Dilthey (1833-1911), Martin Heidegger (1889-1976), Edmund Husserl (1859-1938) na Paul Ricoeur (1913-2005). Miongoni mwao, mtaalamu mwenye mchango mkubwa zaidi katika kuanzisha na kukuza nadharia hii ni Friedrich Schleiermacher (Rutt, 2006).

Msingi wa Nadharia ya Kihemenitiki ni uchunguzi wa matendo mbalimbali ya binadamu kama usemaji, upendaji na uchukiaji. Nadharia hii imejengwa katika imani kwamba matendo na tabia ya binadamu vinaathiriwa kwa njia nyingi na asasi mbalimbali zilizomo katika mazingira yanayomzunguka. Hizi ni asasi za kisiasa, kiutamaduni, kiuchumi na nyinginezo (Wamitila, 2002). Msingi wa nadharia hii unatokana na ukweli kwamba ulimwengu ni mfumo wenye maumbo mengi yanayohusiana (Mkumbwa, 2012). Lengo kuu la nadharia hii ni kuyachunguza mawasiliano pamoja na ufasiri wa maana za matini mbalimbali. Nadharia hii huchunguza jinsi wasomaji wanavyoielewa matini au kazi fulani pamoja na mbinu au njia za uelewaji wenyewe. Makala hii, inaitumia nadharia hii kujadili sababu zilizowafanya waandishi wa kazi teule kuona umuhimu wa kutumia wahusika wa kivisasili katika kazi zao.

Uchunguzi wa kihemenitiki unahusisha hatua tatu muhimu. Hatua ya kwanza ni upitiaji wa matini ili kubaini mbinu mbalimbali za uwasilishaji zilizotumika ndani

ya matini yenyewe. Lengo la hatua hii ni kuona namna maneno yalivyotumiwa na mwandishi katika kuwasilisha ujumbe kwa hadhira yake. Kwa kuzingatia mbinu ya tafsiri ya kisarufi, uwezo wa kufahamu maneno na lugha unatakiwa ili kuelewa maana ya matini. Maneno na sentensi katika aya, kwa jumla, ni lazima vihakikiwe kwa makini ili kupata maana sahihi iliyokusudiwa. Hatuwezi kuelewa maana ya matini nzima bila kuelewa sentensi mojamoja na hata maneno yanayounda sentensi hizo (Palmer, 1969; Stiver, 1996; Delthey, 1996). Hatua ya pili, ni kubaini maana kulingana na maneno, mbinu na maelezo hayo. Hatua ya tatu, ni kufafanua muktadha wa kutumika kwa maneno au mbinu hizo kwa lengo la kubaini ukweli unaobebwa katika mbinu au maneno hayo (Delthey, 1996; Mkumbwa, 2012; Ali na wenzake, 2015). Katika makala hii, tumeitumia Nadharia ya Uhemenitiki huchunguza jinsi kazi teule zinavyoeleweka kwa kupitia wahusika wa kivisasili. Aidha, hatua ya kwanza na ya pili ya nadharia hii zimetuwezesha kuyachunguza mawasiliano ya wahusika hao kisha kufasiri maana ya maneno na maelezo ya wahusika hao. Kwa kufanya hivyo, tumeweza kubaini athari ya matumizi ya wahusika wa kivisasili katika riwaya teule.

## 5.0 Wahusika wa Kivisasili katika Riwaya za *Nagona* na *Mzingile*

Sehemu hii ya makala inajihusisha na ubainishaji wa wahusika wa kivisasili katika riwaya teule. Kabla ya kuwabainisha wahusika hao, kwanza tuone muhtasari wa riwaya teule. Muhtasari wa riwaya ya *Nagona* umeanza na kufuatiwa na muhtasari wa *Mzingile*. Riwaya ya *Nagona* iliandikwa na Euphrase Kezilahabi na kuchapishwa mwaka 1990 na Dar es Salaam University Press (DUP). Riwaya hii inajadili kuhusu maana ya ukweli, maisha, kifo, kuzaliwa na kuwako na kutokuwako. *Nagona* ni riwaya inayothibitisha upevu wa falsafa ya Kezilahabi kuhusu dhana ya maisha. Inaelezea safari ya mhusika mkuu mwanamume asiyetajwa jina akipita katika nchi huku akionekana hajitambui. Mhusika mkuu anajifunza kuhusu "paa wa ajabu" na anaanza kuzifuata nyayo zake ili amkamate. Anatakiwa kuvumbua vitendawili vigumu vilivyowashinda wengi. Anafanikiwa kwa msaada wa wazee wanne wenye nguvu za ajabu. Wazee hao ni nabii, mtume, mfuasi na mtenzi. Riwaya hii inaweza kutazamwa kama pacha wa riwaya ya *Mzingile* kutokana na kushabihiana kwa dhamira zake zinazochambua suala la kifalsafa lihusulo maana ya maisha.

Kwa upande mwingine, riwaya ya *Mzingile* nayo iliandikwa na Euphrase Kezilahabi. Ilichapishwa mwaka 1991 na DUP. Riwaya ya *Mzingile* ni mwendelezo wa riwaya ya *Nagona*. Ilichapishwa mwaka mmoja baada ya riwaya ya *Nagona*. Visa vingi vilivyomo katika *Mzingile* vinaanzia kwenye riwaya ya *Nagona*. Riwaya inajenga maudhui ambayo yamejiegemeza katika visasili vinavyodokezwa kuanzia mwanzo wa riwaya hadi mwisho. Riwaya ya *Mzingile* inahakiki suala la asili na falsafa ya kuchunguza chanzo cha uhai na maarifa. Inatumia motifu ya safari kuonesha mhusika anayetafuta ukweli kuhusu maisha, maana ya dini na maana ya Mungu. Katika safari yake mhusika anaongozwa njia

na msichana ambaye wakati wote wanatengwa na umbali kati yao. Safari yenyewe anaifanya kwa karne nyingi. Baada ya kusafiri kwa muda mrefu na kupitia mambo mengi magumu, anafanikiwa kufika kwa mzee ambaye amejenga nyumba yake juu ya mlima. Mzee huyu anamweleza mambo mengi kuhusu maisha.

Baada ya kuona muhtasari wa vitabu teule, katika sehemu inayofuata tumebainisha wahusika wa kivisasili katika riwaya teule kwa kuanza na riwaya ya *Mzingile*. Katika riwaya hii, Kezilahabi ametumia wahusika wa kivisasili. Kwanza ni mhusika Kakulu ambaye anashabihiana na wahusika wa kiutendi wa fasihi simulizi za Kiafrika. Mfano mzuri wa mhusika wa fasihi simulizi ni mhusika anayepatikana katika *Utenzi wa Nyakiiru Kibi* (1997). Mhusika huyo anaitwa Nyakiiru Kibi. Sifa za wahusika hawa zinafanana na sifa za mhusika wa kivisasili ambazo tumeshazijadili. Mfano mwingine ni ule wa Fumo Liyongo, mhusika anayepatikana katika *Utenzi na Nyimbo za Liyongo* (2006). Vilevile, katika *Utendi wa Mwindo* (1969) wahusika wake wanaafiki madai tunayoyatoa hapa. Tukirudi kwa mhusika Kakulu wa riwaya ya *Mzingile*, wasifu wake wa ndani na wa nje unatuwezesha kuona mbele zaidi ya vile anavyoelezwa katika riwaya. Hata namna anavyozaliwa anatupa picha ya wahusika ambao tumezoea kuwasikia katika fasihi simulizi za Kiafrika. Tukizichunguza hadithi za makabila mbalimbali ya Kiafrika tunakutana na wahusika wenye tabia kama za Kakulu. Nukuu ifuatayo inaeleza jinsi mhusika huyu alivyozaliwa:

> Siku ambayo mama yake aliumwa uchungu, aliitwa mkunga mashuhuri kijijini kuja kumhudumia. Mtoto alipotoa kichwa hadi mabegani mkunga alikimbia akipiga makelele. “Sijaona kitu kama hiki!” Kichwa kilichotokeza kilikuwa na ndevu nyingi ndefu, zenye kuchanganyika na mvi. “Umezaa shetani!” Mkunga aliendelea kupiga kelele. Mama kusikia hivyo alistuka akasahau uchungu, akaanza kukimbia amepanua miguu. Alimzalia nje amesimama hali ameshikilia shina la mti. Yasemekana Kakulu alipodondoka alikata kitovu kwa meno yake, akajipangusapangusa yale maji ya utelezi, akawakaripia wanaume waliokuwa karibu, “Ondokenni hapa! Mnachunguliachungulia nini! Hampaswi kuona mwanzo wangu na njia niliyoijia!” (*Mzingile*, kur. 1-2).

Nukuu inaonesha kuwa Kakulu ni mhusika aliyezaliwa akiwa na ndevu na mvi, anaongea mara tu baada ya kuzaliwa, hanyonyi ziwa la mama yake, anazaliwa hali meno yamejaa mdomoni, anajikata kitovu na kujipangusa maji ya utelezi mwenyewe. Hizi ni sifa za mhusika wa kivisasili kama tulivyozieleza awali katika makala hii. Inaaminika kuwa, Kakulu ni zawadi iliyotolewa na miungu kwa jamii. Alikuwa na wajibu muhimu katika jamii ambao alifanikiwa kuukamilisha. Kabla hajaenda kukaa kwenye nyumba yake ndogo juu ya mlima, alirithisha mila, desturi, tamaduni, taratibu za ibada, matambiko, mipaka na historia ya jamii kwa wazee watano wa kila kijiji (*Mzingile*, uk. 5).

Mfano mwingine wa mhusika wa kivisasili katika riwaya ya *Mzingile* ni mhusika ambaye hana jina, Mimi. Kinachotushawishi kuona kuwa mhusika Mimi ni wa kivisasili ni sifa, dhima na mtazamo wake. Kwa hiyo, Mimi ana sifa za mhusika wa kivisasili. Kwanza, anatawaliwa na motifu ya safari. Mhusika anasema, “nilipokuwa naamka nilianza kufikiria safari ndefu iliyokuwa ikinikabili” (*Mzingile*, uk. 9). Japo hakujua mahali pa kuanzia safari yake. Anasema, “safari yangu ilianza asubuhi na mapema wakati ambapo fikira zilikuwa bado kuchoka. Sikujua nielekee upande gani maana hakuna aliyejua kwa hakika mahali alipoishi (*Mzingile*, uk. 10). Inaelekea huu ni mtindo ambao Kezilahabi anapendelea kuutumia katika kuwaumba wahusika wake wa kivisasili, kutokujua wanakoelekea (Senkoro, 1997).

Sababu iliyomfanya mhusika asiye na jina katika *Mzingile* aanzishe safari hiyo inaelezwa kuwa ni kwenda kutoa taarifa za kilio kwa ndugu wa marehemu. Mmojawapo wa ndugu hao ni mzee, baba wa marehemu ambaye, “anaishi kwenye kibanda kidogo mlimani na mara nyingi huwa usingizini. Mlango wa kibanda hicho haujawahi kufunguliwa na kibanda chenyewe hakina dirisha” (*Mzingile*, kur. 9-10). Mhusika anasema, “muda mrefu sasa umepita nikiwa safarini kuwatangazia wanaohusika juu ya kifo chake” (*Mzingile*, uk. 54). Safari yake ilikuwa ndefu kama anavyodhihirisha mwandishi, “najua safari yako bado ndefu sana. Bado kuna kipande cha karne na karne mbele yako” (*Mzingile*, uk. 52).

Safari ya mhusika wa kivisasili huambatana na kupitia mambo mengi magumu na ya hatari, majaribu kutoka kwa wafalme wakatili, majitu, bahari za kutisha, mito ya hatari na miungu (Senkoro, 1997). Katika safari yake hii ndefu, mhusika alikumbana na vikwazo vingi njiani. Kwa mfano, alitembea kwenye milima na mabonde. Haikuwa rahisi kupanda milima hiyo iliyojulikana katika historia na iliyoficha kilichokuwa upande wa pili. Mabonde yalikuwa yenye maporomoko makali yaliyojulikana pia katika historia kwa kudumaza fikra zisizijikwamue. Alivuka milima, mito na mawe hadi alipofika mahali tambarare (*Mzingile*, uk. 10). Pia, alifukuzwa na fisi. Anasema “nilijikuta nimo safarini peke yangu. Fisi walikuwa wakinifuata. Nguvu za kukimbia sikuwa nazo. Nilianguka chini. Fisi walinijia mbio” (*Mzingile*, uk. 41). Halafu, alipita kwenye mlima uliokuwa mgumu kupandika ambao sehemu yake ya chini ilikuwa ni msitu ulioshonana. “Ilibidi kuwa najipenyeza palipokuwa na mwanya. Baada ya msitu huu nilifika sehemu iliyokuwa na miamba ambayo upandaji wake ulikuwa mgumu sana. Ilinichukua karne nyingi kuvuka sehemu hii” (*Mzingile*, uk. 17). Vilevile, mhusika alipita kwenye pango lenye giza nene na kisha kwenye mto wenye maji ya baridi. Anasema, “polepole niliendelea mbele. Maji yaliponifika shingoni miguu ilianza kutetemeka. Nilijihisi nateleza. Ghafla miguu yangu iliinuliwa na mkondo mkali wa maji nikaviringishwa kama pia. Muda wa kupiga kelele sikuupata (*Mzingile*, uk. 41). Isitoshe, mhusika alipita katika bonde la kutisha. Anasema, “baada ya muda mfupi tulianza kushuka bondeni. Bonde lenyewe lilikuwa kubwa na pana.

Lilikuwa kama bonde la ufa. Mteremko ulianza kuwa mkali. Haukuwa mteremko tena bali maporomoko. Wakati mwingine ilitubidi kushikilia matawi ya miti midogomidogo tusiporomoke" (*Mzingile*, uk. 53). Kisha, alichoshwa na jukumu alilopewa la kwenda kutoa taarifa za kilio kwa ndugu wa marehemu. Tumelibaini hili mhusika anaposema, "muda mrefu sasa umepita nikiwa safarini kuwatangazia wanaohusika juu ya kifo chake. Lakini sasa nimechoka. Wazo lenyewe limeanza kuwa jiwe zito juu ya moyo wangu. Kifo chake kinaanza kuingiliana na maisha yangu" (*Mzingile*, uk. 54). Hii inadhihirisha wazi kuwa jukumu alilopewa mhusika lilikuwa zito.

Pamoja na vikwazo, hatari na majaribu aliyokumbana nayo katika safari yake, mhusika alilitekeleza jukumu lake. Mhusika mwenyewe alikusudia kwa moyo wake wote kulitimiza. Anasema, "lazima nimwone huyo Mfadhili wako. Haina maana kupitia vikwazo vyote hivi na kurudi bila chochote" (*Mzingile*, uk. 53). Alifanya hivyo kutokana na msaada aliopata kutoka kwa marafiki. Kupata msaada kutoka kwa marafiki, ni sifa nyingine ya wahusika wa kivisasili. Marafiki humsaidia katika kutimiza azma na malengo ya safari yake. Humpa msaada wakati wa majaribu, vikwazo na mateso yanayompata kama tulivyoona. Marafiki waliomsaidia mhusika asiye na jina ni pamoja na ndege ambaye alimwonesha njia ya kupita alipofika njiapanda tatu. Hilo linajidhihirisha katika nukuu ifuatayo:

> Nilipoachana na milima, nilifika mahali palipokuwa na njia tatu. Moja ilielekea kushoto kwangu ambako niliona vichaka vidogovidogo vikavu. Kulikuwa na nyayo za mtu aliyepita kitambo maana sikuweza kumwona. Mkono wa kulia niliona njia ambayo ilielekea kutopitiwa na watu wa karne hii. Njia hii ilikuwa na majani yaliyoota hadi katikati. Kwa mbali niliona dalili ya moshi uliotokana na moto mdogo. Lakini majani yaliufanya moyo wangu usite. Njia ya tatu ilikuwa mbele yangu. Ilikuwa imezibwa kwa miiba. Nyuma ya miiba hii njia ilionekana kuwa wazi na ilikuwa haikupinda pinda kama zile zingine mbili. Nilisimama kwa muda nikifikiri njia ya kupita. Nilitazama tena miiba na njia iliyokuwa mbele yangu. Niliona ndege mweupe akirukaruka nyuma ya miiba hiyo katikati ya njia. Moyo wa ujasiri, moyo wa udadisi na utundu ulinisukuma mbele. Nilikata shauri kuiondoa ile miiba nikafuata ile njia ya kati alikokuwa huyo ndege. Nilipokuwa namkaribia, aliruka mbele zaidi, akawa ananiongoza njia (*Mzingile*, uk. 11).

Msaada wa ndege uliishia kwenye mto, lakini alipata msaada mwingine kutoka kwa mwanamke. Huyu alimsaidia kuvuka mto na kumwonesha njia baada ya kuvuka mto huo. Mhusika asiye na jina anasema kuwa aliona mtu kama mwanamke amesimama kwa mbali na, yaelekea alikuwa kwa muda wote ule akimtazama. Alipomwona, alitembea mbele polepole. Mhusika anaeleza zaidi kama ifuatavyo:

> Nilipomtazama machoni, alitabasamu. Bila kusema neno aligeuka. Akatembea kuelekea mtoni. Alikunja nguo zake hadi magotini. Polepole alivuka upande mwingine. Akachukua kibuyu kikubwa cha maji, akakiweka kichwani. Alinigeukia na kunielekeza njia kwa mkono wake wa kulia bila kusema neno. Akageuka akaanza safari yake. Upande alionielekeza ndio yeye pia alifuata (*Mzingile*, uk. 13).

Mwanamke alimwongoza njia mpaka walipokaribia kibanda cha mzee alikokuwa anakwenda kutoa taarifa za msiba. Muda wote alikuwa mbele na mhusika alimfuata. Wakati wote palikuwa na umbali kati yao kiasi cha kutoweza kuongea. Wakati mwingine alikuwa akitoweka, hivyo, ilimlazimu mhusika kufuata nyayo zake. Alipokaribia kwenye kibanda cha mzee, mwanamke alitoweka. Alijitokeza tena siku ambayo mhusika alianza safari ya kurudi baada ya kumwona mzee. Aliongoza njia mpaka pale mtoni alipomkuta mwanzoni. Wakapungiana mkono wa kwaheri. Suala la kuongozwa na kuelekezwa kwa mhusika ni sifa ya msingi ya wahusika wa kivisasili.

Baada ya kuachana na mwanamke, mhusika alipata msaada kutoka kwa kipofu. Alimwona kipofu huyo kiasi cha maili moja hivi kutoka njia panda. Alikuwa amekaa kivulini peke yake amepumzika, karibu sana na njia. Alikuwa mwanamume. Alipomkaribia alimwona akitega sikio moja upande wake. Alipomwangalia vizuri alitambua kuwa alikuwa kipofu. Alikuwa ameshikilia fimbo yake mkononi. Alipoacha kusikia hatua za mhusika, kipofu alisema, “najua umesimama na unanitazama. Mimi ni mboni kati ya giza na mwanga. Nilikuwa sikutegemei wakati kama huu. Umefika mapema kidogo, mwendo wenu ulikuwa wa kasi sana” (*Mzingile*, uk. 43). Hii ina maana kwamba kipofu alijua kuhusu safari ya mhusika na mwanamke aliyemwongoza njia, ndio maana anasema, “mwendo wenu ulikuwa wa kasi.” Tena, kipofu anamwambia mhusika kuwa alikuwa akimsubiri:

> “Najua. Ndio maana nakusuburi.”
>
> “Unanisubiri mimi! Ulijua nitapita njia hii?” “Si hivyo tu. Nilijua ungehitaji msaada wangu. Baada ya njia panda hakuna njia nyingine isipokuwa hii. Ila bila msaada unaovuka mipaka ya mwanga ungeweza kupotea njia. Nakuona unatabasamu. Vipi? Tuondoke?” (*Mzingile*, uk. 44).

Kipofu alimwongoza njia kwenda kwa Mzee ambaye nyumba yake ilikuwa imejengwa katikati ya ziwa na ilikuwa inaeleaelea majini. Walipita sehemu nyingi za hatari, kwa mfano, kwenye pango lenye giza nene, kwenye bonde la ufa lenye maporomoko, penye mteremko mkali, kwenye ardhi yenye unyevunyevu wenye ubaridi, kwenye ardhi yenye kubonyea na kwenye matope. Kisha kipofu

akamwambia mhusika kuwa hawezi kuendelea zaidi, ilikuwa lazima mhusika amalizie safari akiwa peke yake. Nukuu ifuatayo inabainisha hayo:

> Tulitembea usawa wa mto kuelekea maji yalikokuwa yanakwenda. Mwishoni alisimama mahali fulani karibu na kitu kilichoonekana kama mti mkubwa. Baada ya kuupapasa nilihisi kuwa ulikuwa mbuyu. "Sitakwenda zaidi. Mwisho wangu ni hapa. Lazima uvuke peke yako. Ila ninakuonya jambo moja. Lazima uwe na ujasiri. Bila ujasiri hutafika uendako. Usijitie kujua. Utanikuta nakusubiri hapa. Haya! Jitose majini!" (*Mzingile*, uk. 43).

Kipofu alimsubiri palepale. Mhusika alipotoka kwa mzee ambaye kipofu anamwita mfadhili wake, alimkuta bado anamsubiri. Alimwongoza njia. Waliachana mahali walipokutana, yaani kwenye mti kando ya njia. Kipofu alikaa tena kwenye mti na mhusika aliendelea na safari ya kurudi nyumbani. Hivyo, ndege, mwanamke na kipofu waliandaliwa na miungu kwa ajili ya kumsaidia mhusika. Kama siyo msaada wao, ingekuwa vigumu kwa mhusika kukamilisha safari na lengo la safari yake.

Kwa upande wa riwaya ya *Nagona*, vilevile Kezilahabi ametumia wahusika wa kivisasili. Mhusika wa kwanza wa kivisasili katika riwaya ya *Nagona* anaitwa mhusika jumui, anayepatikana katika *Nagona* na *Mzingile* tu. Ni mhusika wengi katika mmoja (Madumulla, 2009: 137). Anaitwa pia mhusika "mimi" ambaye ana *Id, Ego* na *Superego* ndani yake (*Nagona*, uk. 31). Mhusika huyu ameletwa na Kezilahabi kwa mara ya kwanza katika fasihi ya Kiswahili. Hajampata mfuasi bado. Huenda ni katika bunilizi zake za kimajaribio ambapo William Mkufya na kitabu chake cha *Ziraili na Zirani* ameelekea kupiga hatua kubwa kumfuata (Madumulla, 2009: 140).

Mhusika "mimi" katika *Nagona* ni wa kivisasili. Sifa za mhusika wa kivisasili zinazojibainisha kwa mhusika huyu ni nyingi. Kwanza, maisha yake yanaambatana na motifu ya safari ambapo mhusika aliondoka nyumbani na kusafiri kwenda mbali. Sababu za kufanya safari hiyo ilikuwa ni kwenda kumsaka paa. "Mimi nimo safarini. Ninamfuata paa. Nilikuwa nikifuatilia nyayo zake. Lakini nilipofika hapa niliona maluweluwe nyayo zikanipotea. Mnaweza kunielekeza alipoelekea?" (*Nagona*, uk. 48). Sifa ya pili, ni kwamba katika safari yake alikumbana na mambo mengi magumu na ya hatari. Alipata majaribu na vikwazo vingi kutoka kwa mfalme kabla ya kufanikiwa kumpata paa aliyekuwa anamtafuta. Vikwazo vingi alivyokumbana navyo akiwa njiani, vingine alivipata alipofika kwenye jumba la mfalme ambamo paa alikuwa akiishi. Kwa mfano, alipewa kazi nne za kufanya kama mtihani kwake. Alitakiwa kufuzu mtihani huo ili aweze kukabidhiwa paa.

Kazi walizopewa zilikuwa ngumu. Watu wengi waliofika kwenye jumba la mfalme walishindwa kuzifanya kutokana na huo ugumu. Mfalme aliwaaambia, “kabla sijawapa huyo mumsakaye, kuna kazi ambazo nataka mnifanyie. Kazi ya kwanza, nina shamba langu dogo. Nataka lilimwe leo hii hii lote. Si kubwa nendeni” (*Nagona*, uk. 56). Waliongozwa na msichana aliyewekwa maalumu kwa ajili ya kuwapa maelekezo. Walipofika shambani waliinua majembe kwa nguvu zao zote na kushusha. Lakini ardhi ilikuwa ngumu na jembe halikuingia udongoni hata robo inchi. Hapakuwa na uwezekano wa kumaliza shamba hilo kwa muda wa siku moja (*Nagona*, uk. 57).

Kazi ya pili ilikuwa ni kuusukuma mlima ambao ulikuwa unamkinga mfalme asipate mwanga wa jua la asubuhi. Mfalme alikuwa mzee, alihitaji mwanga wa jua ili kuondoa baridi ya asubuhi. Hivyo, alitaka wausukume kidogo mlima huo na walitakiwa kukamilisha kazi hiyo kabla ya mapambazuko (*Nagona*, uk. 57). Kazi ya tatu, mfalme alitaka kiko chake kirudishwe. Alikisahau kiko hicho alipokwenda kumtembelea mfalme mwenzake wa nchi ya Sibara. Umbali wa kutoka kwenye jumba la mfalme walipokuwapo hadi kwenye nchi hiyo ya Sibara ilikuwa ni mwendo wa miaka saba (*Nagona*, uk. 58). Kazi ya mwisho ilikuwa ni kucheza bao na paa. Aliwaambia, “paa mnayemtaka anajua sana kucheza bao. Nataka acheze na mmoja kati yenu. Katika ufalme huu hakuna anayeweza kumshinda” (*Nagona*, uk. 58). Haya yalikuwa ni majaribu magumu kwa mhusika “mimi”, hapakuwa na uwezekano wa kuyashinda peke yake. Hata mwandishi mwenyewe anakiri kwamba mhusika alipitia mambo magumu anaposema: “usiwe na haraka, kuna vikwazo vingi, lakini kushinda vikwazo ni kuifikia kweli. Safari ni ndefu, lakini kusafiri si kufika. Jambo muhimu ni kufikiri” (*Nagona*, uk. 42).

Ili kuhakikisha kwamba anashinda vikwazo na majaribu ya njiani, mhusika huyu alipewa marafiki. Hii ni sifa nyingine ya wahusika wa kivisasili. Mhusika katika kusafiri kwake anakutana na marafiki wanaomuunga mkono na kumsaidia katika kutimiza azma na malengo ya safari yake. Marafiki hao humpa msaada wakati wa majaribu, vikwazo na mateso yanayompata. Wakati mwingine anaweza kupata msaada na maelekezo muhimu kuhusu safari yake kutoka kwa miungu wa kike au wa kiume (Belcher, 1999).

Marafiki aliowapata ni wazee wanne, ambao ni Mtenzi mkausha maji, Mtume mhamisha milima, Mfuasi mwenye mguu mrefu na Nabii mcheza bao, ushindi ukapatikana. Mtenzi alimsaidia “mimi” kufanya kazi ya kwanza ya kulima shamba. Walipokuwa karibu wakate tamaa kulima lile shamba, mtenzi mkausha maji aliinama akatapika maji aliyokunywa mtoni. Ardhi iliyokuwa na kiu iliyanyonya maji kwa hamu kubwa, udongo ukawa tope, wakaanza kulima (*Nagona*, uk. 57). Wangekatwa vichwa kama siyo msaada wa Mtenzi. Mtume alisogeza mlima. Walikuwa wameshaandaa shingo zao kwa shoka kali kama si Mtume kuwaokoa (*Nagona*, kur. 57-58). Mfuasi alirudisha kiko cha mfalme kwa

kuukunjua mguu wake mrefu kuelekea upande wa kaskazini. Alitumia muda mfupi kufanya hivyo (*Nagona*, kur. 58-59). Nabii alicheza bao na paa na kumshinda. Walikabidhiwa paa baada ya kushinda vikwazo vyote.

Watu walijua habari za "mimi" hata kabla ya kumwona. Walipomwona hawakushangaa, walisema kuwa walikuwa wanamsubiri tena kwa miaka mingi na walijua kuwa atapita. Hii ina maana kwamba walikuwa wameshaambiwa kuhusu mhusika huyu na wajibu ambao alipaswa kuufanya. Kwa mfano, mhusika "mimi" alipokutana na Nabii na Mtume kwa mara ya kwanza walimwambia:

> Utusamehe macho yetu yana ukungu. Lakini sasa tumekutambua. Wewe ndiye tukusubiriye. "Yaelekea ndiye yeye". Yule mzee wa pili alisema, "tazama macho yake, yaelekea kuona mbali. Na tazama kichwa chake kinaelekea kufikiri". Tumekuwa tukikusubiri. Huu sasa ni mwaka wa elfu mbili. Bado hatujakata tamaa tulijua utafika. "Tazama alivyo! Alama zote anazo! Upinde na mshale! Ndiye yeye! Ndiye yeye" (*Nagona*, uk. 45).

Pia, habari za kusubiriwa kwa mhusika huyu zinatajwa katika kurasa za 42, 48, 50 na 53.

Mhusika mwingine wa kivisasili anapatika katika riwaya ya *Nagona* ukurasa wa 35 ambapo mwandishi anasimulia kuhusu kisasili cha mfalme Edipode. Mwandishi anaeleza kuhusu mhusika kizee, anasema:

> Nilitaka tu kuwaonesha mahali kitendawili kilipoanzia. Kizee kilisimama karibu na mti mkubwa. Kilitazama juu ya mti huo, kikasema kikielekeza mkongoja kwenye shina, yasemekana kitendawili kilianzia hapa (*Nagona*, uk. 35).

Uteuzi wa mhusika alioufanya mwandishi unasawiri wahusika wa kivisasili. Mara nyingi katika hadithi simulizi anayesimulia hadithi ni kizee, ambaye anaweza kuwa babu au bibi. Katika nukuu tunaona kuwa kizee kinasimulia kisasili cha mfalme Edipode.

## 6.0 Wahusika wa Kivisasili katika riwaya ya *Ziraili na Zirani*

Kwa upande wa riwaya ya *Ziraili na Zirani*, mhusika wa kwanza wa kivisasili ni Ziraili. Huyu ni mhusika ambaye anaonekana kujihusisha na maandiko matakatifu na hekima za kale, na anatumika kuunganisha visasili na uhalisia. Mhusika kama huyu tunampata katika tamthiliya ya *Aliyeonja Pepo* (1974) ya Farouk Topan. Katika tamthiliya hii ya *Aliyeonja Pepo*, mhusika Ziraili anajitokeza kuanzia onesho la kwanza hadi la mwisho. Tukirudi kwenye riwaya ya *Ziraili na Zirani*, Zirani ni mhusika mwingine wa kivisasili katika riwaya hii. Huyu ni mhusika muhimu katika riwaya hii, siyo tu kwa sababu ya jina lake ambalo linamaanisha

'kuzira' au 'kususia', na nafasi anayocheza, bali pia kwa sababu ya kurejelea kwenye dhana ya visasili.

Dhana ya visasili katika riwaya inawaweka wahusika wa riwaya husika katika mtazamo mpya. Inavutia kujadili uhusika wa Zirani, kwa mfano, kwa mtazamo wa kujitoa kwake katika kutekeleza majukumu yake. Mwanzoni anaonekana kuwajibika sana katika nafasi yake lakini anapowekwa katika mazingira tofauti anabadilika. Migogoro kati ya Ziraili na Zirani ambayo ndiyo inaweka msingi wa riwaya yenyewe ina muundo wa kivisasili. Hata kabla mwandishi hajatukutanisha na Zirani, tunahisi mchango wake kwa kimya kwamba aliumiza akili za malaika wengi akiwamo Ziraili. Tendo lake la kwanza ni kutoroka katika koba la Ziraili wakati akipelekwa kuzimu. Kitendo hicho kinatafsiriwa kama ishara ya kudharau patakatifu pa patakatifu au uasi (Wamitila, 2002).

Mhusika mwingine wa kivisasili anayepatikana katika riwaya ya *Ziraili na Zirani* anaitwa Kinjeketile Ngwale. Tukumbuke kuwa katika riwaya hii kuna matukio ya kweli ambayo yamesukwa pamoja na matukio ya kubuni ili kuipa hadithi vionjo. Hali kadhalika, wahusika wa riwaya hii ni mchanganyiko wa wahusika wa kubuni na wale wa kihistoria. Mulokozi (1990) akieleza kuhusu wahusika wa riwaya ya kihistoria anasema "tunaweza kuwagawa wahusika katika makundi matatu. Kundi ka kwanza ni la watu maarufu. Kwa mfano, Mirambo na Chaka. Kundi la pili ni la watu wasiofahamika sana. Kwa mfano, wasaidizi au watumishi wa viongozi wakubwa.

Kundi la tatu ni la watu wanaopewa sifa za kubuni, yaani ruwaza za kisanaa ingawa walikuwapo kihistoria. Wahusika wa namna hii tunawakuta katika tendi simulizi kama vile, Sunjata, Liondo na Rukiza" (Mulokozi, 1990: 3). Tunaweza kumweka mhusika Kinjeketile katika kundi la tatu. Kwa sababu, Kinjeketile Ngwale ni mhusika ambaye pamoja na kwamba mwandishi amemfinyanga kisanaa, aliishi kweli katika historia ya nchi yetu. Kinjeketile Ngwale alikuwa kiongozi wa Vita vya Majimaji vilivyotokea mwaka 1905 hadi 1907 (Masuha, 2008). Vita vya Majimaji ni mapigano makali ya Waafrika katika Tanganyika Kusini dhidi ya utawala wa kikoloni katika koloni la Ujerumani ndani ya Afrika Mashariki. Vita hivyo vililenga kumkomboa Mtanzania kutoka mikononi mwa Wajerumani (Menda, 2006). Wapiganaji walipewa dawa ambayo ilisadikiwa kuwa ingeweza kugeuza risasi kuwa maji. Kinjeketile na wenzake walifanikiwa kuchoma maboma ya Wajerumani baada ya kwenda huko usiku. Dawa ya majimaji iliaminiwa kuwa inafaa baada ya kujaribiwa katika eneo la Songea. Kinjeketile Ngwale alikuwa mwanzilishi wa dawa hiyo pamoja na vita vyenyewe vya Majimaji.

Ujitokezaji wa mhusika huyu umejiegemeza katika uwapo wa kisasili cha Vita vya Majimaji katika riwaya ya *Ziraili na Zirani*.

## 7.0 Athari ya Wahusika wa Kivisasili katika Riwaya Teule

Wahusika wa kivisasili wana athari zifuatazo katika riwaya teule:

### 7.1 Urithishaji wa Amali za Kiutamaduni na Uhistorishaji

Makala hii imebaini kwamba kutumika kwa wahusika wa kivisasili katika riwaya teule kumebeba lengo la kuonesha asili, chanzo na namna mambo yalivyo ndani ya jamii.

Katika kueleza mlolongo wa matukio na matokeo yake, wahusika hao huibua historia ya jamii na kuiwezesha kutafakari ilikotoka, ilipo sasa na kule inakokwenda na kutathmini kuhusiana na namna inavyoweza kujiendeleza vizuri zaidi katika nyanja za siasa, utamaduni, uchumi na mahusiano (Mkumbwa, 2012). Kwa mujibu wa Frye (1973), jukumu la kuhifadhi amali za jamii linaonekana kuligusa zaidi kundi la waandishi wa fasihi kuliko makundi mengine ya wanajamii. Hivyo, waandishi wa riwaya teule, kupitia wahusika wa kivisasili, wanakusudia kuhifadhi baadhi ya amali za jadi kwa kutumia kazi zao. Frye (1973) anatuambia kwamba dunia inashuhudia mwendo wa haraka sana kuelekea maendeleo na matumizi makubwa ya sayansi na teknolojia katika shughuli mbalimbali. Kwa kadiri tunavyosonga mbele, ndivyo mambo ya kijadi yanavyozidi kubadilika sura yake na mengine kupotea kabisa. Katika hali kama hii, kuendelea kushikilia njia moja pekee ya kutunza amali hizi za jamii ni kupoteza urithi wa thamani. Amali nyingi za jamii zinahifadhiwa vizuri zaidi ndani ya hadithi zilizoandikwa na simulizi za kijadi (Frye, 1973: 139,140).

Kwa sababu hiyo, makala hii imebaini kwamba kuwapo kwa mwingiliano mkubwa wa kijamii, kumewafanya baadhi ya waandishi wa riwaya kuona kuwa wana jukumu la kuzitunza amali za kifasihi ili zisipotee kabisa. Kwa hiyo, wanatumia wahusika wa kivisasili katika riwaya zao ili kuhifadhi na kurithisha amali hizo kwa vizazi vijavyo. Okpewho (1980) anaweka uzito kwenye hoja hii anaposema kuwa visasili ambavyo hubeba wahusika wa kivisasili, vimetumika ili kurithisha amali na kutunza historia ya jamii. Anaeleza kwamba visasili vina mamlaka ya kuonesha historia ya mtu au ya jamii, kwa hiyo, visichukuliwe kwa uhafifu kama kwamba kazi yake ni kuleta fantasia pekee.

Pia, riwaya ni kama dafina au ghala ya kuhifadhi amali mbalimbali za kijamii. Hii inatokana na sifa yake ya upana wa mawanda. Riwaya ina uwezo wa kuhifadhi historia ya jamii. Mwandishi ni kama karani ambaye anafanya kazi ya kutunza historia ya nchi yake kwa njia ya kazi zake za kifasihi (Madumulla, 2009). Utunzaji wa historia ya nchi anaouzungumzia Madumulla, hufanywa kwa kutumia wahuska wa kivisasili. Mathalani, katika riwaya ya *Ziraili na Zirani*, mwandishi, kwa kutumia wahusika wa kivisasili, ameweza kurithisha amali za kiutamaduni na kuhifadhi kumbukumbu za kale. Kumbukumbu zilizohifadhiwa ni kama vile: asili

ya binadamu ambapo inaaminika kuwa ni Mungu mwenyewe aliyewaumba wanadamu wa kwanza, Adamu na mkewe, Hawa. Pia, kumbukumbu kuhusu asili ya Amri Kumi za Mungu kwa waumini wa dini za Kikristo na Kiislamu, Amri ambazo zinasadikiwa kuwa alipewa Musa alipopanda katika mlima Sinai. Vilevile, kuna historia ya mnara wa Babeli ambao ndio ulikuwa asili ya makabila na lugha duniani. Historia hiyo inahifadhiwa na kurithishwa kutoka kizazi hadi kizazi. Aidha, kuna kumbukumbu kuhusu historia ya gharika iliyoangamiza kila kitu isipokuwa Nuhu na familia yake. Pia, wanyama, ndege na wadudu waliangamia isipokuwa jozi ya wawiliwawili ambao Mungu alimwagiza Nuhu kuwaweka kwenye safina.

Katika riwaya ya *Mzingile* kupitia mhusika Kakulu, tunaona kuwa riwaya imesheheni mafunzo mengi kuhusu mila na desturi, dawa za asili, unajimu na historia ya nchi. Kakulu alionesha mfano wa kurithisha maarifa yote haya kwa mzee mmojammoja kutoka katika vijiji vitano, baada ya kuona kuwa amezeeka. Wajibu wa wazee hao ilikuwa ni kuhifadhi, kudumisha na kurithisha ujuzi na maarifa hayo kwa vizazi na vizazi katika vijiji vyao. Hivyo, mhusika huyu, anasaidia kuhifadhi kumbukumbu ya matambiko na miviga iliyokuwa inafanywa na mababu zetu zamani za kale. Kwa jinsi mila na desturi zinavyobadilika kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia, kumbukumbu kama hizi ni muhimu kuwako kwa ajili ya vizazi vya sasa na vinavyokuja. Nukuu hii inaweka uzito kwenye maelezo hayo:

> Yasemekana Kakulu alipojiona mzee, aliwateua wazee watano, mmoja kutoka kila kijiji akaenda nao msituni. Huko alikaa nao kwa muda wa mwezi mmoja, akiwafunza historia, mila na desturi, dawa, unajimu na mengine mengi. Alipoona wamekomaa aliwaongoza hadi chini ya mlima mkubwa. Alipanda nao hadi kwenye kilele cha mlima. Kwa mara ya kwanza wakaiona nyumba yake ndogo. Walipokuwa juu ya mlima aliwaonesha kwa fimbo yake nchi iliyokuwa chini. "Hii yote ni nchi yenu msikubali ichukuliwe na watu wageni" (*Mzingile*, uk. 5).

Hapa tunaona kuwa baada ya Kakulu kuzeeka sana aliamua kurithisha ujuzi wa dawa za asili, unajimu, utamaduni na historia aliyokuwa nayo kuhusu jamii kwa wazee wengine. Kwa hiyo, kwa kutumia mhusika wa kivisasili, Kakulu, historia inahifadhiwa.

### 7.2 Kuunganisha Ujadi na Usasa

Mwandishi amewatumia wahusika wa kivisasili, Kakulu, katika riwaya ya *Mzingile* na, Kinjeketile Ngwale, katika *Ziraili na Zirani* kuonesha jinsi wahusika wa aina hii wanavyotumiwa kuunganisha ukale na usasa. Mwandishi kwa kumtumia mhusika Kakulu, kwa mfano, anaeleza kuhusu umuhimu wa misitu ambamo hapo zamani matambiko yalikuwa yanafanywa. Pia, anataja miungu ambao hapo kale waliheshimika katika jamii lakini katika kizazi cha leo nafasi na

heshima kwao imepungua kutokana na jamii kukumbwa na maendeleo ya sayansi na teknolojia pamoja na dini za kigeni na utandawazi. Kwa hiyo, waandishi wanapochanganya matumizi ya wahusika wa kivisasili ndani ya riwaya, wanafanya mchanganyiko wa ukale au asili na usasa. Visasili ni hazina ya maarifa, maadili, na falsafa za jamii ambazo hufasiriwa upya kulingana na mahitaji ya kisasa. Kupitia visasili, jamii inahifadhi historia na utambulisho wake huku ikijifunza kuishi kwa hekima katika dunia inayoendelea kubadilika. Ni kiungo kinachounganisha fikra za mababu na mitazamo ya kisasa, hivyo, kuhakikisha kuwa urithi wa kale unaendelea kuwa hai katika maisha ya leo. Kwa njia hii, visasili vinathibitisha kwamba ukale si kikwazo cha maendeleo, bali ni msingi wa usasa. Hivyo, visasili si tu masimulizi ya kale, bali ni daraja hai linalounganisha vizazi, tamaduni na mitazamo kati ya wakati wa jana na wa leo.

**7.3 Kutambulisha Jamii**

Wahusika wa kivisasili waliotumika katika riwaya teule wanaweza kuangaliwa kama kipengele muhimu katika suala zima la utambulisho. Kwa kutumia wahusika hawa, utambulisho unarahisishwa, ni njia mojawapo ya kuonesha jinsi utambulisho wetu ulivyofungamana na kiini cha wahusika hawa.

Wahusika wa kivisasili wana mchango mkubwa sana katika kutuelekeza kifikira kwamba tungali tunauthamini utamaduni wetu. Kwa vyovyote vile, utamaduni huu hatuwezi kuukwepa katika shughuli zetu, hata shughuli za sanaa zinazohitaji ubunifu.

Kwa kuendelea kutumia mbinu hii ya kifasihi simulizi, tunaendelea kujitambulisha sisi ni nani. Uandishi wa namna hii, kwa kiwango kikubwa, unatutaka tuanze kujisaili wenyewe. Pamoja na kwamba sisi tunadhani kuwa tumeendelea sana kiteknolojia, lakini pia kuna utambulisho wetu. Ni vizuri kuamua kufanya jitihada za kimakusudi kuuenzi utambulisho wetu. Kwa hiyo, ili kurudi katika utamaduni wetu, inabidi tutumie kile tunachokifahamu. Tusipoufahamu utamaduni wetu inatuwia vigumu kuzielewa kazi zinazotumia visasili na tanzu nyingine za fasihi simulizi ndani yake.

Naye Mkufya (Mahojiano tarehe 17/09/2013) ana mtazamo mpana zaidi kuhusu suala la visasili na utambulisho wa Mwafrika. Anadadavua kuwa alianza kujikita katika udadisi wa mambo ya dini kuanzia mwaka 1966 akiwa na umri wa miaka 15. Anasema aliupinga Ukristo na wakati huo huo hakuwa na mpango wa kujiunga na Uislamu. Kuanzia wakati huo amekuwa akifanya udadisi wa masuala ya kidini kwa muda mrefu hata kabla ya kuandika *The Wicked Walk* (1977).

Akieleza kuhusu riwaya yake, Mkufya anasema kuwa *Ziraili na Zirani* aliiandika ili kuzima kiu ya kujibu mapigo. Anasema, riwaya nyingi zikiwamo za *Paradise Lost* (1667) na *Pilgrims Progress* (1678) zinaonekana kuwa na mwelekeo wa kuupendelea Ukristo. Ukisoma hekaya za Wayunani nyingi zinapendelea namna

Wayunani na Warumi wanavyoyatazama mambo ya ulimwengu na hatima ya mtu akishakwenda mautini. Lakini kwa Mwafrika kuna pengo. Kwa nini hadithi na hekaya za Mwafrika zisipewe nafasi na kuheshimiwa kama za Wayunani na Warumi. Kwa hiyo, *Ziraili na Zirani* ni riwaya yenye tamko, hoja na kauli ambazo zinapingana na zile zilizomo katika *Paradise Lost* (1667), *Pilgrims Progress* (1678) na riwaya nyingine zinazotetea sana dini za watu weupe.

Mkufya anadhihirisha hayo katika *Ziraili na Zirani* anapoonesha msisitizo wa kuheshimu dini ya asili za Kiafrika. Anamtumia mhusika Kinjeketile Ngwale kutuonesha jinsi alivyosimama kidete kutetea dini za asili za Kiafrika baada ya mhusika Rahabu kudhihaki imani yake. Rahabu anamwambia Kinjeketile:

> Na wewe mfuasi wa Bokelo uliyejaa madonda ya dharuba za kuzimu pia wataka kuichokoza pepo. Unadhani moto wake waweza kupozwa kwa mnyunyo wa maji? Oi! Huruma wee! Eti shetani twaungana na kiroja cha hawa mazebe waliozinduliwa toka kwenye giza la jadi zao haramu na misitu ya kuchomea nyama za vibudu! Yeye aliyewakaribisha washamba hawa kuzimu, hakika anastahili kuzimwa!" Ngwale akajibu: "Niondokee shetani mwovu! Tena usidiriki kijihusisha na misitu ya mizimu yetu tunayoienzi na kuitambikia! Akuhusishaye wewe na mizimu yetu ni mpumbavu, mshamba asiyekujua wewe vizuri na asiye mstarabu wa kutaka kutujua sisi (*Ziraili na Zirani*, uk. 182).

Wakati Mkufya anamwita Mungu aliyeabudiwa na mhusika Kinjeketile, Bokelo, Ebrahimu Hussein katika tamthiliya yake ya *Kinjeketile* (1969) anatumia miungu wawili ambao ni Kolelo na Hongo. Inaaminika na watu wengi kuwa miungu hawa ndio waliompa Kinjekitile (wa kweli katika historia) wazo la kupigana vita kwa kutumia maji.

**8.0 Hitimisho**

Makala hii imeonesha athari ya wahusika wa kivisasili katika riwaya ya Kiswahili. Jumla ya riwaya zilizotumika ni tatu, mbili za Euphrase Kezilahabi za *Nagona* na *Mzingile* na riwaya moja ya William Mkufya ya *Ziraili na Zirani*. Riwaya teule zilizochunguzwa zimedhihirisha kuwa zimesheheni wahusika wa kivisasili ambao wana athari kubwa katika riwaya teule na riwaya ya Kiswahili kwa jumla. Nadharia ya Uhemenitiki imetuwezesha kujadili athari za wahusika wa kivisasili katika riwaya. Katika makala hii imebainika kwamba mojawapo ya athari hizo ni urithishaji wa amali za kiutamaduni na uhistorishaji ambapo imeonekana kuwa riwaya ni njia mojawapo ya kuhifadhi, kutunza na kurithisha amali za jamii. Kwa hiyo, katika makala hii tumeona kuwa riwaya inachukuliwa kama dafina au ghala la kuhifadhi amali mbalimbali za kijamii. Hii ni kutokana na sifa ya riwaya ya kuwa na mawanda mapana. Aidha, imebainika kuwa wahusika wa kivisasili wanapotumika ndani ya riwaya, wanabeba athari ya uunganishaji wa ujadi na

usasa ambapo masuala ya kijadi na ya kikale yanaibuliwa kwa upya katika kizazi cha sasa. Kwa kutumia wahusika hawa, tumebaini umuhimu wa masuala yaliyokuwa yanafanyika kale na umuhimu wake katika jamii, masuala hayo ni pamoja na matambiko. Pia, katika makala haya tumejadili kuwa wahusika wa kivisasili wanabeba athari ya utambulishaji wa jamii husika.

**Marejeleo**

Ali, M.A.M., Usman, A.H., Kadir, M.N.A., Nazri, A. na Faizulamri, M. (2015) "Hermeneutics in the Eye of Al Ghazali." *Mediterranean Journal of Social Sciences*, Juz. 6(4 S2): 39-45.

Bal, M. (1997) *Narratology: Introduction to the Theory of Narrative* (Toleo la 2). Toronto: University of Toronto Press.

Bascom, W.R. (1965) The Form of Folklore: Prose Narratives. *The Journal of American Folklore*, Juz. 78: 1-19.

Belcher, S. (1999). *Epic Traditions of Africa.* Bloomington: Indiana University Press.

Bowra, C.M. (1952) *Heroic Poetry.* London: Macmillan.

Delthey, W. (1996) *Schleiermacher's Hermeneutical System in Relation to Earlier Protestant Hermeneutics*. Princeton: Princeton University Press.

Frye, N. (1957) *Anatomy of Criticism.* New Jersey: Princeton University Press.

Kasper, K. na Wuckel, D. (1982) *Grundbegriffe der Literaturanalyse*. Leipzig: VEBBibliographisches Institut Leipzig.

Magoulick, M. (2000) "Characteristics of Myth". Inapatikana katika https://facult.gcsu.edu/custom-website/mary-magoulick/mythmagicmordenworld. Iliseomwa tarehe 10 Julai 2024.

Menda, A. (2006) "Kinjekitile Ngwale na Historia yenye Utata". *Tanzania Daima.* 21 Septemba 2006. uk. 7.

Mkumbwa, A. (2012) *Ujitokezaji wa Visasili na Visakale katika Riwaya ya Kiswahili ya Majaribio*. Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Msokile, M. (1992) *Kunga za Fasihi na Lugha*. Dar es Salaam: Educational Publishers and Distributors Ltd.

Murray, H.A. (1960) *Myth and Mythmaking.* New York: George Braziller, Inc.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999) *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Okpewho, I. (1992) *African Oral Literature: Backgrounds, Character and Continuity.* Bloomington: Indiana University Press.

Palmer, R.E. (1969a) *Hermeneutics.* Evanston: Northwestern University Press.

__________ (1969b) *Hermeneutics: Interpretation Theory in Schleiermacher, Dilthey, Heidegger and Gadamer*. Illinois: Northwestern University Press.

Senkoro, F.E.M.K. (1997) *The Significance of the Journey in Folk Tales from Zanzibar*. Tasinifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

__________ (1982) *Riwaya ya Kiswahili*. Dar es Salaam: DUP.

Stiver, D.R. (1996) *The Philosophy of Religious Language.* Oxford: Blackwell Publishers Ltd.

Sungi, N.A. (2011) *Ruwaza ya Shujaa Mwanamke wa Kiutendi katika Jamii ya Wanyanyembe wa Tabora*. Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Rutt, J. (2006) On Hermeneutics. Inapatikana katika www.mcser.org Ilisomwa tarehe 02 Agosti 2024.

Wamitila, K.W. (2003) *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi : Focus Books.

__________(2002) *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake.* Nairobi: Phoenix Publishers.

Yerushalmi, Y.H. (1982) *Jewish History and Jewish Memory*. London: University of Washington Press.